

MATUMAINI PROG NO:2382

TITLE: HOW TO BE A REAL CHRISTIAN

SUMMARY: KINAANGAZIA KUHUSU NJIA ILIYO SAHIHI YA KUFANYIKA KUWA MKRISTO KAMILI.

TEXT: WAEFESO 4:1-6

MADA: NAMNA YA KUWA MKRISTO HALISI

.....

Hujambo mpendwa popote tunapopatana huku nikiwa nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuunganika pamoja nami tena kupitia kwa upendo Wake Mwenyezi Mungu ili tukajifunze kutoka kwenye neno Lake.

Nakukaribisha katika kipindi hiki cha Matumaini kutoka TWR Nairobi.

Natumai ya kwamba, tangu wakati wa Mwisho kupatana nawe, ungali mzima katika Bwana.

Leo hii pia tunaendelea na mafundisho yetu kutoka kwenye Waraka huu wa mtume Paulo kwa sura yake ya nne kuanzia aya yake ya kwanza hadi ile ya sita (Waefeso 4:1-6)

Katika waraka huu, mtume Paulo anazumzia kuhusu njia ya kufanyika kuwa Mtu ambaye ni Mkristo Halisi.

Tutakapo fika ukingoni mwa somo leo,,, mpendwa,,nitakuwa nashiriki nawe anwani yangu kwa sababu ya mawasiliano kati yetu pamoja nawe.

Mimi naitwa Vincent Amara nikiiwa kwa utanguliza nawakaribisha watumishi Guardian Angel na Esther Musila na wimbo Liko lango .

WIMBO:

Ni Guardian Angel na Esther Musila na wimbo lango. Na ni kweli kaisa Lango la mbinguni li wazi na nikupitia kwa Yesu Kristo.....

OMBI. Mfalme wa Ajabu tena Baba yetu wa Mbinguni. Tunasema ni asante kwa sababu ya kutufanyia lango wazi kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Tusaidie kulielewa somo la leo kuhusu namna ya kufanyika kuwa Wakristo halisi...ni kwa Yesu tumeomba ...----Amen

Karibu tena katika kipindi hiki cha Matumaini kutoka TWR ambapo leo hii tunajifunza kuhusu njia ya kufanyika kuwa Mkristo halisi huku ujumbe wetu tukiutoa kwenye Waraka wa Mtume Paulo kwa Waefeso 4:1-6.

Mpendwa kama tujuavyo ni kwamba,,hamna yeyote miongoni mwetu ambaye amanpenda mtu asiye kuwa mwaaminifu. Sisi hata kidogo hatuwapendi watu hao ambao hujifanya kuwa wazuri kabisa ili hali siavyo.

Ninao uhakika ya kwamba,,hata wewe mwenyewe humpenda tu ambaye ni mnyoofu na tabia yake ya ndani na nje zinaandamana kabisa.

Katika ulimwengu humu tunamoishi,,utakuta ya kwamba watu wengi sana wanaishi kwa njia ya uwongo na kuuficha ukweli wao.

Rafiki yangu,,hebu nikueleze ya kwamba,,, kuwa mtu ambaye ni halisi au wa uhakika,,, kunahitaji jitihada ya hali ya juu zaidi. Vile vile,,kuwa Mkristo halisi kunahitaji zaidi ya jitihada.

Na kwambia hivi ya kwamba,,,kuwa Mkristo halisi kunahitaji msaada kutoka kwa Mungu.

Ningependa nikuonyeshe jinsi unavyoweza kupokea msaada huo kutoka kwa Mungu katika ujumbe huu ambao nimeupa mada,,**jinsi ya kuwa Mkristo halisi.**

Katika waraka huu wa Mtume Paulo kwa Waefeso sura yake ya 4:1-6,,tunataka kuona jinsi ambavyo aliwaandikia na kuwaeleza kuhusu changamoto za kiroho pamoja na vipimo vyake ili kufanyika kuwa Wakristo halisi.

Nasoma;

1. Basi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, nawasihi mwenende kama inavyoustahili wito mlioitiwa;

2. Kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukulia katika upendo;
3. Kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani.
4. Kuna mwili mmoja, na Roho mmoja, kama vile mliyoyitwa katika tumaini moja la wito wenu;
5. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja,
6. Mungu mmoja na Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.

Dada yangu,,ili kuelewa Wakristo halisi ni nini, tunapaswa kuyachunguza **maombi** kadhaa ambayo Mtume Paulo ameyasema katika fungu hili la neno.

Jambo la kwanza kabisa,,tunaambiwa ya kwamba,,**Wakristo halisi au ukipenda wa kweli watatembea kwa namna unavyostahili wito wao.**

Katika kayaanza mafundisho haya,,tunamwoona Mtume Paulo akitumia neno “kusihi”. Maana nyingine ya neno hili ‘kushisi’ ni Kuomba au pia kuhimiza. Bila shaka msikilizaji wangu Neno hili nilenye nguvu sana na linahitaji hatua kwa wale wanaosikiliza au wale waliokuwa wakiisoma barua yake.

Mtume anaendelea kusema hivi, “Mnaenenda kama inavyostahili wito mlioitiwa?” Kwa hiyo kustahili kunamaanisha kufaa au kulingana na inavyopaswa kuwa.

Ndugu yangu,,kama tunavyoona hapa ni kwamba,,Wito wa Mkristo unatoka Kwake Mwenyezi Mungu. Sisi kama Wakristo tunapaswa kuwa watu ambao ni wa kuvimilia na zaidi wenye kunyenyekea kwa upole.

Kwa hivyo Mkristo halisi anapaswa kutembea kulingana na wito wake. Wakristo wanaotembea kwa uangalifu hawaonyeshi tu jinsi Mkristo anavyopaswa kuishi bali humfurahisha Mungu. Bila shaka hivyo ndivyo sote tunatamani kufanya.

Jambo la pili ni kwamba,,**wakristo halisi watahifadhi umoja wa roho.**

Kunalo Neno hili kujitahidi ambalo maana yake ni, “kufanya kila juhudi,,kuwa na bidii au pia kujaribu kwa bidii,” ili kuweka umoja wa Roho. Sasa naona kwamba hakusema jaribuni sana kuunda umoja wa Roho au

kuzalisha umoja wa Roho. Badala yake anasema tujitahidi sana kudumisha umoja wa Roho. Hiyo inamaanisha kuilinda na kuihifadhi, sio kuizalisha, sio kuiunda. Bila shaka rafiki,,,Roho ndiye anayeleta umoja umoja wa Roho.

Kwa hiyo Mtume anawahimiza wasomaji wake kwamba Wakristo halisi wataweka umoja wa Roho. Wakristo wa kweli hulinda, kutunza, na kuhifadhi huo umoja wa Roho kwa amani.

Jambo la tatu na la mwisho ambalo tunaloangalia kwa leo kuhusiana na wito wa Mtume ni kwamba,,,WAKRISTO HALISI WATAONA UMOJA WA WITO WAO.

Tunapoiangazia mistari ya 4, 5, na 6, tunamwoona Mtume akiwa anaorodhesha umoja huo kwa mara saba. Malengo ya umwoja huo,,ni kutuelekeza namana ambavyo sisi kama Wakristo tunapaswa kuutunza.

Anasema kuna mwili mmoja. Na kuna ushirika mmoja mkuu. Hii ina maana ya kwamba,,Wakristo wote wa kweli ni sehemu ya mwili mmoja mkuu.

Kisha Mtume anasema kuna Roho mmoja. Hii ikiwa na maana ya kwamba Roho mtakatifu anayewaunganisha watu.

Kwa wakati wa Sasa kunayo roho ya kugawanya ambayo ni roho ya shetani aliye adui ya kila mmoja wetu.

Mtume anaendelea na kusema kuna tumaini moja la wito wako. Ameandika,, Mmeitwa katika tumaini moja la wito wenu.

Rafiki yangu,,Tumaini hilo moja hukaa au kutulia ndani ya Yesu Kristo Ambaye ndiye Msingi wa tumaini hilo.

Katika aya ya tano,, anaseama ya kwamba,,kuna Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja,

Msikilizaji wangu,,ni vyema kujua ya kwamba Lengo la imani yetu kama Wakristo ni Yesu Kristo Pekee. . Kisha akasema kuna ubatizo mmoja. Kwa hili anamaanisha ubatizo ambao ni jibu la dhamiri njema kwa Mungu.

Kisha katika aya ya 6 anamalizia hivi: "Mungu mmoja na Baba wa wote, aliye juu ya yote, na katika yote na ndani ya yote." Hebu fikiria kulihusu hilo . Mungu wetu anapatikana kote na hata pale ulipo kwa sasa.

Mtume Paulo, akizungumza huko Athene, aliwaambia watu hao wa Kigiriki kwamba Mungu hayuko mbali na yeyote kati yao.

Mpendwa,,kama ambavyo tumejifunza kwa leo,,tumeona ya kwamba,,Wakristo wa kweli huwa na umoja kwa njia ya mwili mmoja, Roho mmoja, tumaini moja, Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja, Mungu mmoja na Baba wa wote. Bwana asifiwe!

Rafiki yangu,,Sisi kama Wakristo tunaweza kupungukiwa na maombi haya ambayo Mtume Paulo anayaweka mbele yetu,,walakini kwa neema ya Mungu tutayazitimiza kwa neema ya Mungu. Narudia tena ya kwamba,,sisi kama Wakristo hatuwezi Pekee yetu. Sisi Wakristo tunapaswa kutembea katika wito wetu ,,tunapaswa kuweka umoja wa Kiroho. Hatimae ni kwamba tunapaswa kuuona umoja wetu katika Mwenyezi Mungu.

Kwa msaada zaidi,,wacha tuwasiliane kwa anwani nitakayo kushirikisha hapo baadae.

OMBI.. Mfalme wa Wafalme Uliye inuliwa juu ya vyote.Tunakushukuru kwa somo hili la leo kuhusu namna ya kufanyika kuwa Wakristo halisi.Tuma Roho Wakio akatuongoze katika kulifanikisha na,,,ni kwa Kikristo tumeomba.....Amen.....

Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu.Kipindi cha matumaini kutoka Twr. Leo tumejifunza kuhusu **Namna ya kuwa Mkristo halisi.**

Ujumbe wetu tumeutoa kwenye kitabu cha Waefeso 4:1-6.

Iwapo umeweza kubarikiwa, au anacho kitu ambacho ungependwa kusema nasi au hata maswali ya Bibilia, tafadhali zungumza nasi kupitia kwa anwani nitakayoshiriki nawe baada ya wimbo huu Niwezeshe naye dada yetu Amnobe Pilipili

WIMBO.....

Ni dada yetu Amnobe Pilipili ,...na wimbo Niwezeshe.....

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2

Barua Pepe-barua@twr.co.ke